



Hakika kundi la kwanza la watu watakaoingia peponi watakuwa katika sura ya mwezi usiku wa tarehe kumi na tano, kisha wale wanaowafuata watakuwa katika sura ya nyota kali ing'aayo na iangazayo mbinguni

Kutoka kwa Abuu Huraira -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-: "Hakika kundi la kwanza la watu watakaoingia peponi watakuwa katika sura ya mwezi usiku wa tarehe kumi na tano, kisha wale wanaowafuata watakuwa katika sura ya nyota kali ing'aayo na iangazayo mbinguni, hawatokwenda haja ndogo wala kubwa, na wala hawatotema mate wala kupenga kamasi, vitana vyao vitakuwa vya dhahabu, jasho lao litakuwa ni miski, na vitezo vyao vitakuwa vikinukia udi wenye harufu nzuri mno, udi wa marashi, na wake zao watakuwa ni katika Mahurulaini, na wote watakuwa katika umbile la mtu mmoja, watakuwa katika sura ya baba yao Adam, urefu kwenda juu ni dhiraal sitini (Dhiraal moja ni inchi 18)".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa kundi la kwanza la waumini watakaoingia peponi nyuso zao zitakuwa na sura ya mwezi unapokuwa usiku wa tarehe kumi na tano katika mg'ao, kisha wale wanaowafuata watakuwa katika sura ya nyota kali yenye mng'ao na mwangaza katika mbingu, watakuwa na sifa za ukamilifu kiasi kwamba hawatokojoa, wala kujisaidia haja kubwa, na wala hawatotema mate wala kupenga kamasi, vitana vyao ni vya dhahabu, na jasho lao ni miski, na vitezo vyao vitakuwa vinafuka hurufu nzuri mno, na udi mzuri zaidi, na wake zao watakuwa ni Mahurulaini, umbile lao litakuwa kama umbile la mtu mmoja, watakuwa katika sura ya baba yao Adam katika urefu na umbile; ulikuwa urefu wa mwili wake ni dhiraal sitini kwenda juu.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/65183>

